



VITUO ATAMIZI VYA KILIMOBIAHARA VYA AIC TANGAZO KWA VIJANA FURSA YA KUJIUNGA 2020/21

Kituo cha Ubunifu wa Kilimobiashara (AIC), ambacho ni idara ya Taasisi ya PASS inapenda kuwatangazia vijana wenye nia ya kufanya kilimobiashara kwamba kinapokea maombi ya kujiunga na Vituo Atamizi vya Kilimobiashara vilivyopo SUA Morogoro na TALIRI Farm, Mbande, Kongwa mkoani Dodoma.

Katika vituo hivi, AIC inawapa fursa vijana ya kuanzisha, kumiliki na kuendesha kilimobiashara kwenye sekta ndogo ya mboga na matunda na mifugo na nyama.

Kijana atakayeomba nafasi hii anatakiwa awe na tabia njema, mtiifu, mwenye nidhamu, mchapakazi, fikra chanya, mwaminifu na anayependa kuona matokeo chanya. Vijana wa Kike watapewa Kipaumbele.

Vijana washiriki kwenye Vituo Atamizi watapewa vifaa, miundo mbinu, na mtaji wa kufanya kilimobiashara ambapo watausimamia kwa kipindi cha miezi 12.

Katika kipindi chote, waatainiwa watapewa usimamizi wa karibu ikiwemo ushauri wa kibiasara na upelembaji, ili kuhakikisha wanafanikiwa katika shughuli zao za kilimobiashara.

Baada ya kukamilika kwa muda huo, vijana watakaofanikiwa kwenye kilimobiashara, AIC itawawezesha kufanikisha kuanzisha biashara kama hiyo kwenye maeneo yao.

Vijana wenye nia wanashauriwa kutuma maombi yao ya kujiunga na kituo Atamizi kimojawapo kati ya SUA-AIC Morogoro kinachojihusisha na kilimobiashara cha mboga na

matunda au AIC Kongwa kilichopo Taliri Farm (PRC), Mbande, Kongwa kinachojihusisha na biashara ya unenepeshaji/ufugaji mbuzi na usindikaji wa nyama ya mbuzi. Vijana 280 watachaguliwa kwenye awamu ya kwanza ya mchujo (200 kwa kituo cha Morogoro na 80 kwa Kituo cha Kongwa) na kati ya hawa, vijana 140 (100 Morogoro and 40 Kongwa) watachaguliwa kwenye awamu ya pili ya mchujo kujiunga na Vituo Atamizi kuanzia Oktoba 2020.

Kwa maelezo zaidi na jinsi ya kupata, kujaza na kurudisha fomu ya maombi yanapatikana kwenye tovuti ya www.aic.co.tz na www.pass.or.tz, SUA-SAEBS, ofisi za AIC (SUA, Morogoro na Mbande, Kongwa) na ofisi zote za PASS nchini.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 30/06/2020 saa 11.00 jioni.

